Wananchi wana haki ya kupata nyaraka na vielelezo mbalimbali toka serikalini kwa ajili ya kuruhusu ufanisi katika usimamizi bora wa shughuli za umma!

Wasiliana nasi:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu
Legal and Human Rights Centre [LHRC]
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
Simu: +255 22 2773038/48; Nukushi: +255 22 2773037
Barua Pepe: lhrc@humanrights.or.tz
Tovuti: www.humanrights.or.tz

Ofisi ya Arusha
Barabara ya Engira, Kitalu Na. 48
S. L. P. 15243 - Arusha
Simu: +255 27 2544187
Barua Pepe: lhrcarusha@humanrights.or.tz

Kituo cha Msaada wa Sheria
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633 - Dar es Salaam
Simu/Nukushi: +255 22 2761205/6
Barua Pepe: legalaid@humanrights.or.tz

Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi - OGP

...kukuza uwazi, kuongeza ushiriki wa wananchi, kupambana na rushwa, na kuunganisha teknolojia mpya na kuifanya serikali kuwa wazi zaidi, kuongeza ufanisi, na uwajibikaji.

Kimeandaliwa na:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu [LHRC]
Jengo la Jaji Lugakingira
Kijitonyama – Dar es Salaam
S. L. P. 75254
Simu: +255 22 2773038/48 Nukushi: +255 22 2773037
Barua Pepe: lhrc@humanrights.or.tz
Tovuti: www.humanrights.or.tz

UTAMBULISHO WA KITUO

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1995, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kimekua kwa kasi sambamba na maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini. Kituo hiki kinafanya kazi nchi nzima kupitia mipango yake ya huduma za mafunzo kwa jamii na ufuatiliaji wa ukiukwaji wa haki za binadamu. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina ushawishi wa mabadiliko ya sera, sheria na taratibu mbalimbali katika ngazi ya kitaifa kwa kupata nguvu na uhalali wa kuyatenda hayo kutoka kwa jamii.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Makampuni, sura ya 212 ya sheria za Tanzania kama shirika lisilo la serikali, la kujitolea na lisilo jitafutia faida kwa nia ya kugawana.

Shirika hili liliundwa kutokana na mradi wa haki za binadamu wa Shirika la Mpango wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania [TANLET]. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina makao yake makuu jijini Dar es Salaam na ofisi ndogo mkoani Arusha.

Maono

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye HAKI na USAWA.

za afya zilizo mbali na kliniki kwa kuboresha upatikanaji wa huduma za matibabu ili kuokoa maisha na kushughulikia mambo ya dharura yanayoibuka katika jamii za vijijini. Mpango huu unalenga utoaji wa huduma maalumu ya afya. Kwasasa, huduma za ***telemedicine*** zinatolewa na Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) iliyopo Dar es Salaam kwa kushirikiana na hospitali 10 zilizopo nchini India.

Kuanzishwa kwa Sekta ya mfumo wa usimamizi wa habari za maji (wsmis) zinazojumuisha mifumo ya ramani ya maji kama chombo cha mipango na ufuatiliaji wa huduma za usambazaji maji; na

Kuanzishwa kwa shirika la Kielektroniki la Serikali (eGA), taasisi yenye ubunifu wa kusimamia, kuratibu na kukuza matumizi ya TEKNOHAMA (ICT) ili kuboresha utoaji wa huduma.

Utungaji wa Sheria ya Matumizi ya Chaguzi ya mwaka 2010 ili kutekeleza uwajibikaji kwenye fedha kwa vyama vya kisiasa. Sheria hii imelenga kudhibiti matumizi ya fedha zaidi ya vizingiti vinavyotolewa na kukabilana na vitendo vya rushwa kwenye chaguzi tofauti.

TEKNOLOJIA NA UBUNIFU

Kuidhinishwa kwa Sera ya Kitaifa ya habari na teknolojia ya mawasiliano (ICT) ya mwaka 2003 imeweka jukwaa la kuibadilisha Tanzania kuwa taifa lenye misingi ya maarifa/elimu. Sera hii imekuwa msingi wa idara za Serikali, taasisi za elimu, mashirika yasiyo ya kiserikali na wajasiriamali tofauti kupata ufumbuzi wa ICT ili kusaidia utoaji wa huduma. Baadhi ya mifumo ya utoaji wa huduma ambayo inafanya kazi kwa sasa ni; Mifumo ya usimazi wa fedha, mifumo ya kitaifa ya ulipaji mishahara, mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu, tovuti na mifumo ya sekta maalum ya misaada.

Kuanzishwa kwa Mpango wa maendeleo ya Tanzania zaidi ya kesho (Tanzania Beyond Tomorrow) mpango wa elimu ya kielektroniki. Mpango huu unalenga katika maendeleo ya elimu ya kielektroniki katika mashule, vyuo vya elimu ya watu wazima na mashirika ya elimu zisizokuwa rasmi.

Kuanzishwa kwa huduma bora za madawa ***(telemedicine)*** kwa kulenga utoaji wa huduma

Tamko la Lengo Mahsusi

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali, lisilo la kutafuta faida kwa nia ya kugawana, lisilo na fungamano na chama chochote cha siasa, linalojibidisha kujenga uwezo wa jamii, kulinda, kutetea na kupigania haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

Maadili ya Shirika

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinaamini katika maadili ambayo hutoa mwongozo wa jinsi wanachama wake, bodi ya wakurugenzi, wafanyakazi na wadau wengine wanavyopaswa kuenenda. Maadili hayo ni kama yafuatayo:

- Uadilifu;
- Usawa;
- Uwazi;
- Uwajibikaji;
- Weledi; na
- Kujitoa na Kujitolea.

UTANGULIZI

Mpango wa kimataifa wa kuendesha shughuli za serikali kwa uwazi ulizinduliwa mwaka 2011 kama jukwaa la kimataifa la wanamageuzi wa ndani ya nchi ili kuzifanya serikali zao ziwe na; uwazi, uwajibikaji, na usikivu kwa wananchi wake. Toka kuanzishwa kwake, OGP imekua kutoka nchi 8 hadi kufikia nchi 62 na Tanzania ikiwemo. Katika nchi hizi zoye, serikali na Asasi za Kiraia zinapaswa kufanya kazi pamoja ili kuendeleza na kutekeleza mageuzi ya wazi ya kiserikali.

DHAMIRA YA SERIKALI YA TANZANIA KATIKA MPANGO WA KIMATAIFA WA KUENDESHA SHUGHULI ZA SERIKALI KWA UWAZI (OGP)

UWAZI

Kuanzishwa kwa kamati angalizi tatu za Bunge zikiwa na wenyeviti ambao watatoka katika vyama vya upinzania ili kuangalia matumizi ya Serikali yanayohusiana na rasilimali zilizopo katika Serikali kuu, serikali za mitaa na mashirika ya umma.

Uanzishaji wa masanduku ya maoni katika wizara tofauti, kurugenzi tofauti na mamlaka tofauti, ofisi za serikali kuu na serikali za mitaa zinazokusudiwa kuwa na kazi za kusikiliza malalamiko, maoni na kuchukua maoni kutoka kwa umma.

miongo miwili (miaka 20) iliyopita hasa kuelekea mwishoni mwa miaka ya 90, Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa za uwajibishaji na uadilishaji ili kupingana na rushwa na kuendeleza mifumo ya upokeaji. Hatua zilizochukuliwa ni:

Uanzishwaji wa Mpango wa kitaifa wa Kupinga Rushwa (NACSAP) mwaka 1999. Mpango huo unatoa mwongozo ndani ya MDAs, Mikoa na Serikali za Mitaa zinazotakiwa kuanzisha hatua madhubuti za kuelezea rushwa ndani ya maeneo waliyomo na mamlaka ya kisheria. Kamati ya NACSAP ilianzishwa kwa kupata wanachama kutoka Serikalini na nje ya serikali ili kuhakikisha utekelezaji wa mkakati.

Uanzishaji wa mfumo wa Ufuatiliaji wa ukaguzi wa Matumizi ya umma ambapo Serikali kwa ushirikiano wa vyama vya kiraia juu ya utekelezaji wa bajeti na kukadiria kiasi cha thamani ya pesa.(sentesi si kamilifu).

Uanzishaji wa njia inayohusiana na utoaji wa mifumo ya ugawaji unaorahisisha ugawaji wa rasilimali kwa serikali za mitaa kwa njia zilizo wazi. Njia hii itatumika kugawanya rasilimali kulingana na makundi tofauti kama vile sense, upatikanaji wa wa huduma za kijamii, umaskini, namba na eneo la ardhi.

kijiji kwa mtu binafsi au mashirika au wabia waliowasilisha maombi kwenye serikali za vijiji. Kwa mujibu wa na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, viongozi wote hawajatoa amri/maagizo ya kugawa ardhi. Vijiji vyenye kujali jinsia na mabaraza ya ardhi yameanzishwa kusuluhisha migogoro ya ardhi**.**

Ushirikishaji wa wananchi na wadau kwenye utungaji wa sera au sheria ili kupata mawazo na maoni kabla hazijapitishwa na Bunge.

Uanzishaji mtandao wa kitaifa (CLK Net) utakaokuwa jukwaa la kutoa fursa za kupokea mambo mbalimbali kutoka kwa umma/wananchi ili kuendeleza sera za maendeleo na tafakari.

UWAJIBIKAJI NA UAMINIFU

Wakati wa uzinduzi wa Bunge jipya la 2005, Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete alisisitiza juu ya umuhimu wa uadilifu kwa wafanyakazi wa umma:… ***"…Naiomba kamati ya tume ya maadili kwa wafanyakazi wa umma kutokuwa na aibu kuulizana juu ya kila mtu kuweka wazi mali na utajiri wake. Tume inatakiwa kuchukua tahadhari. Nitaisaidia kuijengea uwezo wa kufanya kazi hiyo kama utahitajika kama hilo ni tatizo."*** Kwa zaidi ya

Uanzishaji wa mamlaka ya udhibiti na ununuzi ya umma (PPRA) kuhakikisha kuwa shughuli zote za ununuzi zinafanywa kulingana na Sheria ya Ununuzi**.** Sheria hii inataka kati ya mambo mbalimbali kuwepo na utangazaji wa zabuni kwenye magazeti na tovuti.

Kujiunga na Mfumo wa Kiafrika wa uchunguzi mwenza (African Peer Review Mechanism (APRM) mwaka 2004, uanzishaji wa mkakati wa kujikadiria wa Bara la Afrika katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na ushirika wa umma.

KUHUSISHA WANANCHI

Ushirikishaji wa wananchi unahakikisha ushikirishaji wa wana jamiii katika kufanya maamuzi kwenye mambo yanayowaathiri au katika mambo ambayo wana maslahi nayo. Ushirikishaji wa wananchi unaongeza uhalalishaji wa shughuli za serikali nje ya mipaka ya nchi. Wananchi lazima wahisi wanahusishwa katika serikali, wanahusishwa katika kufanya maamuzi kwa manufaa yao, wawe na uwezo wa kutoa mawazo yao kuhusiana na ufanisi wa Serikali na lazima watambue iwapo mawazo yao yanapewa nafasi kabla maamuzi hayajafanyika na kwa sababu wao ndio wanufaika wa maamuzi hayo.

Serikali imeanzisha mikakati mbalimbali kuhakikisha kwamba wananchi wanahusishwa kwenye shughuli zake za kila siku. Mikakati

hii imeanzishwa katika ngazi zote za shughuli za Serikali ingawaje kuna changamoto kadhaa ambazo hazijawasilishwa ili kuongeza ushirikishwaji hasa maeneo ya vijijini.

Mikakati iliyoanzishwa kuhakikisha wananchi wanahusishwa ni pamoja na:

Uanzishaji wa tovuti mwaka 2007 ili kuwawezesha wananchi kutoa maoni yao, kuuliza maswali na kupata majibu kutoka Serikalini.

Uundaji na upitishwaji wa bajeti za serikali za mitaa kwa kutumia mtazamo shirikishi ujulikanao kama Fursa na Vizuizi/Vikwazo kwa Maendeleo. ("Opportunities and Obstacles Development" (O&OD).) Mtazamo huu huruhusu vijiji kutayarisha mipango na kuiwasilisha kwenye ngazi ya juu ya Serikali za Mitaa ili iwekwe kwenye mipango na bajeti za halmashauri.

Uanzishaji/uundaji wa utaratibu wa kufanya mazungumzo ya sekta zinazohusiana na serikali, vyama vya kijamii, sekta binafsi na washirika wa kimaendeleo uliolenga kuboresha/kuongeza matokeo madhubuti na yanayotakiwa katika utekelezaji wa sekta za programu za maendeleo.

Moja kati ya kazi ya mazungumzo ya sekta ni kufanya uchunguzi/uangalizi wa pamoja

wa mwaka ambapo, taarifa za ufanisi wa mwaka wa sekta zinawasilishwa na mambo yanayopewa kipaumbele kwa mwaka unaofuata kama ilivyojadiliwa na kukubaliwa.

Uanzishaji wa mazungumzo ya uangalizi wa matumizi ya umma (Public Expenditure Review {PER}). Uangalizi wa matumizi ya umma ni mazungumzo ya hali ya juu baina ya Serikali, washirika wa maendeleo, na vyama vya kijamii, lakini pia ni baraza la kiufundi ambapo Serikali hutumia kupata mawazo/maoni kwa ajili ya kuendeleza upangaji, utengenezaji wa bajeti na usimamizi wa fedha.

Uanzishaji wa mazungumzo ya sera ya mwaka kutafakari/kuangalia matumizi ya umma, bajeti ya kutegemeza ya ujumla (General Budget Support (GBS)) na Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Hili ni tukio moja linaloshirikisha watu wapatao 1,000 kutoka Serikalini, Asasi za kiraia, sekta binafsi, washirika wa kimaendeleo na mashirika ya kidini ambapo michango inayotokana na mijadala itaingizwa kwenye mpango wa taifa na mfumo wa bajeti.

Ufunguzi wa mifumo ya wazi ya ugawaji wa ardhi za vijiji unaotaka Mabaraza ya Vijiji kupitisha azimio la kugawa ardhi ya